



MAOMBI YA TAARIFA YA KUONYESHA NIA KWA AJILI YA UTOAJI HUDUMA ZA KIBENKI (UFUNGUZI WA AKAUNTI NA USIMAMIZI) KWA AJILI YA MRADI WA BOMBA LA MAFUTA GHAFI LA AFRIKA MASHARIKI (EACOP) – KUMBUKUMBU NA. 10006553

TOTAL East Africa Midstream B.V (Kampuni) Tanzania, kampuni ya Mafuta na Gesi, inaalki makapuni yenye uzoefu na sifa kutuma nia ya kutoa huduma za muhimu kwa ajili ya ufunguzi wa akaunti za benki kwa Waguswa wanaostahiki kupokea fidia pamoja na usimamizi wa malipo ya fidia za kifedha kwa ajili ya Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP).

Mradi wa EACOP unajumuisha ujenzi na uendeshaji wa bomba la kusafirisha Mafuta linalokatisha mipaka ya nchi mbili na litakalo safirisha Mafuta kutoka eneo la Ziwa Albert nchini Uganda mpaka pwni ya Mashariki ya Tanzania kwa ajili ya kusafirisha Mafuta katika masoko ya kimataifa. Bomba litaanzia Kabaale katika Wilaya ya Hoima, nchini Uganda, mpaka Chongoleani, Mkoa wa Tanga nchini Tanzania. Urefu wa bomba ni kilomita 1,443, kati yake kilomita 1,147 zitakuwa nchini Tanzania. Eneo la bomba katika upande wa Tanzania litakafiza Mikoa nane (8), ikiwemo Kagera, Geita, Shinyanga, Tabora, Singida, Dodoma, Manyara na Tanga. Bomba litapita katika Mamlaka za Halmashauri za Wilaya 27 na Vijiji 231.

MAELEZO MAFUPI YA HUDUMA:

Mradi unahitaji mkuza/uchororo katika ardhini na Miundombinu ya Juu ya Ardhini (AGI's) kwa ajili ya ujenzi na uendeshaji wa bomba la Mafuta. Utaaji wa ardhini unahitaji malipo ya fidia kulingana na mfumo mzima wa sheria za Tanzania na Mipango Kazi ya Uhamishaji wa Watu na Makazi ya Mradi.

Kampuni inahitaji huduma za Taasisi za Benki/Fedha kutoa huduma kwa ajili ya kazi za:

- Ufunguzi wa akaunti za benki kwa Kaya takribani 9,000 pamoja na usimamizi wa akaunti hizo katika Mikoa nane (8).
- Mafunzo kuhusu akaunti za benki na elimu ya kifedha kama vile kuhusu uwekaji fedha katika akaunti, utoaji fedha, usimamizi wa akiba ya fedha, michakato ya kibenki inayoendana na huduma hizi

za fedha, vigezo pamoja na matumizi ya mashine mbalimbali za fedha na huduma za mawakala wa benki.

- Malipo ya fidia na Ushahidi wa malipo kwa kushirikiana na Kampuni.

Kazi hii itahitaji uwepo wa wafanyakazi wa MKANDARASI atakayechaguliwa katika eneo husika (uwandani) pamoja na ushirikishaji kaya wa ana kwa ana chini ya usimamizi na mwongozo wa mfunyakazi wa KAMPUNI.

VIGEZO MUHIMU:

Makampuni yanayonyesha nia yanaalkiwa kutuma maombi pamoja na nyaraka zifuatazo:

- Uthibitisho wa usajili wa Benki/Taasisi ya Fedha chini ya Sheria za Tanzania.
- Uthibitisho wa usajili wa Mamlaka ya Mapato ya Tanzania (TRA) na Cheti cha Ithibati ya Malipo ya Kodi cha mwaka wa hivi karibuni.
- Orodha ya matawi ya benki na/au wakala wa benki katika Wilaya zilizopitwa na Bomba la Mafuta -Misenyi, Bukoba, Muleba, Biharamulo, Chato, Geita, Bukombe, Mbogwe, Halmashauri ya Mji wa Kahama, Nzega, Halmashauri ya Mji wa Nzega, Igunga, Wilaya ya Singida, Mkalama, Iramba, Wilaya ya Kondoa, Chemba, Kiteto, Hanang', Kilindi, Wilaya ya Handeni, Halmashauri ya Mji wa Handeni, Korogwe, Muheza na Halmashauri ya Mji wa Tanga.
- Maelezo kwa ufupi ya uzoefu wa ufunguzi wa akaunti za benki, malipo na usimamizi wa huduma kwa ajili ya malipo ya fidia ya miradi mikubwa ya miundombinu nchini Tanzania hadi kufikia jamii zilizo vijijini.
- Msimamizi anayependekezwa atakayefanya kazi katika huu Mradi pamoja na uzoefu wake katika kutoa huduma kama hizi.

Makampuni yenye nia, ambayo yana uwezo na rasilimali za kutoa huduma zilizotajwa hapo juu zinatakiwa kutuma taarifa ya kuonyesha nia iliyoandaliwa kwa lugha ya kingereza pamoja na nyaraka tajwa kupitia barua pepe: talal.mufti@external.total.com (ukubwa usiozidi MB20) hadi kufikia saa 11:00 jioni Majira ya Afrika Mashariki, tarehe **Friday 12th Februari 2021**.

Muhimu: Kwa ajili ya kutengeneza orodha ya makampuni ya Awali yenye vigezo, Mradi wa EACOP utapitia na kuchambua nyaraka zilizotumwa na makampuni yenye nia. Mwaliko kwa Makampuni kutuma maombi ya zabuni utatumwa kwa Makampuni ya Awali yenye vigezo baada ya makampuni hayo kusaini Makubaliano ya Utunzaji wa Taarifa (NDA).